# OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO

*MAWASIANO YA SIMU*:
1. 0755 083 649
2. 0762 281 200

**SHULE YA SEKONDARI NASULI**
**S. L. P. 21,**
**NAMTUMBO**

30/03/2022.

KUMB.NA.NSS/S.30/2/VOL.1/10
JINA LA MWANAFUNZI………………………………
S. L. P ……………………,
____________________.

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NASULI KIDATO CHA TANO 2022/2023**

**1.0: UTANGULIZI**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022/2023. Shule hii ipo kilometa 68 mashariki mwa mji mkuu wa mkoa wa Ruvuma (Songea) na Kilometa 185 magharibi mwa wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

Usafiri wa Basi toka Songea mjini unapatikana kituo cha Mabasi Songea, nauli ni Tshs 3,500/=. Ukifika Namtumbo teremka katika kituo kikuu cha mabasi cha Namtumbo na shule yetu ipo upande wa pili wa barabara. UNATAKIWA KURIPOTI SHULENI KUANZIA TAREHE ITAKAYOTANGAZWA NA WIZARA KWA MHULA WA KWANZA WA MASOMO.

Mwanafunzi atakaechelewa kuripoti kwa tarehe hiyo, nafasi yake atapewa mwanafunzi mwengine.

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1. SARE ZA SHULE**

i. Shati nyeupe mbili mikono mifupi (Mashati mawili au zaidi)
ii. Sketi ya rangi ya Kijani iliyoiva (dark green) yenye rinda box mbele na nyuma yenye urefu Sentimita 15 toka unyayoni (**Sketi fupi HAZIKUBALIKI)**.
iii. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
iv. Soksi nyeupe (jozi mbili).
v. Sweta la shule rangi ya kijani iliyoiva(dark green).
vi. Nguo za kushindia, (Shamba dress) ni Gauni rangi ya damu yam zee, mshono ni solo. Gauni liwe na urefu wa sintimeta 15 kutoka unyayoni.
vii. Hijabu ifanane na sare za shule (Nyeupe na Damu ya mzee sio mtandio isiwe na urembo wala lessi).
viii. Kwa waislamu nguo ya msikitini ni
-suruali dark blue ya heshima na isibane
-nusu kanzu ndefu ipite magoti na yenye mikono mirefu
ix. Sare ya michezo, traksuit nyeusi zenye michirizi nyeupe pembeni na raba nyeupe.
x. Tshirt zinapatikana shuleni kwa Tshs 15,000/=

**2.2. MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA MWANAFUNZI**

i. Madaftari yasiyopungua 10 quire three kwa ajili ya kutunzia notes na daftari aina yoyote kwa ajili ya mazoezi kwa kila somo.
ii. Mkebe wenye vifaa vya mahesabu.
iii. Kalamu za wino bluu/nyeusi, rula ndefu (sentimita 30), kalamu ya risasi,graph pad 04 kwa mwaka,ream 02 kwa mwaka yaani 01 kila mhula, faili 01 kwa ajiliya kutunzia nyaraka

zake,scientific calculator kwa wanaosoma masomo ya sayansi, dissecting kit(kwa wanaosoma Biology) na koti la maabara jeupe ( kwa wanaosoma CBG na PCB)

iv. Aje na sanduku(sanduku la bati ) linalofunga vizuri kwa ajili ya kuhifadhia nguo zake na vitu vyake.

v. Aje na godoro la futi $2^{1}/^{2}$ kwa futi 6 pamoja na mto na foronya yake

vi. Aje na blanketi 01,shuka rangi ya bluu bahari 02,pinki 01, chandarua rangi nyeupe/bluu 01 na taulo 01.

vii. Aje na kifaa kimoja(01) kulingana na mkondo wake kama ifuatavyo:
- HGL-Jembe jipya lenye mpini 01
- HGE-kwanja 01
- PCB- panga 01
- CBG- reki 01

viii. Fagio (chelewa) 02 na soft bloom 01, hard bloom 01na brashi ngumu 01yenye mpini mfupi kwa ajili ya kusafishia sinki la choo

ix. Ndoo ya lita kumi mbili (02) na Squeezer 01 kwa ajili ya kukaushia maji sakafuni

x. Aje na matokeo ya kidato cha nne (result slip) na cheti cha kuzaliwa.

**2.4. AFYA**

Fomu ya kupimwa Afya imeambatanishwa, hakikisha umepimwa sio kujaza tu. Tatizo lolote la kiafya kinyume na vipimo vya daktari shule haitahusika. Fomu hii iletwe shuleni siku ya kuripoti mwanafunzi.

**2.5. FOMU YA KUKUBALI KUTEKELEZA WAJIBU NA TAARIFA BINAFSI**

Fomu hii imeambatanishwa. Ijazwe vizuri na iletwe shuleni siku ya kuripoti.

**3.0: ADA NA MICHANGO**

a) Ada ya shule ni Shilingi 70,000/= kwa mwaka, unatakiwa kulipa shilingi 35,000/= kwa muhula, fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **62401100009 Jina la akaunti (NASULI SECONDARY SCHOOL) benki ya NMB** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye karatasi ya kuwekea hela (paying slip) na iletwe shuleni siku atakayoripoti mwanafunzi.

b) **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni kama ifuatavyo:-**

**(i).** Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
**(ii).** Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
**(iii).** Shilingi 6,000/= kwa ajili ya picha na kitambulisho
**(iv).** Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
**(v).** Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza
**(vi).** Shilingi 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima
**(vii).** Shilingi 5,000/= kwa ajili ya tahadhari (Haitarejeshwa)
**(viii).** Aje na Tsh 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya kwa mwaka mzima (kwa wale ambao hawana bima ya afya). Ni muhimu sana kwani itamsaidia kutibiwa kwa mwaka mzima sehemu yoyote nchini.(fedha hizo siyo sehemu ya michango ya shule, hivyo alete fedha taslimu. Asiingize kwenye akaunti ya shule)

*Michango hii pia ilipwe katika akaunti ya shule iliyotajwa hapo juu.*

***N:B: Jumla ya Ada na michango kwa mwaka ni 176,000/=***

**4.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule ina endeshwa kwa mujibu wa sheria za wizara ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayo tolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu chini ya ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia

mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

**a)** Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
**b)** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
**c)** Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (night preparation)
**d)** Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
**e)** Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
**f)** Kutunza mali binafsi na mali ya umma.
**g)** Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
**h)** Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa ikiwa pamoja na wakati kwenda nyumbani likizo na wakati wa kurudi shule kutoka nyumbani na nje ya eneo la shule muda wowote hata akiwa katika ruhusa.
**i)** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
**j)** Mwanafunzi awe na nywele fupi- njiti ya kiberiti ikichomekwa ionekane. Haruhusiwi kusuka nywele.
**k)** Mwanafunzi ni lazima akumbuke kuwa ni marufuku sare ya shule kuvaliwa pamoja na vitu vifuatavyo:
- Kofia
- Hereni
- Bangili
- Viatu vya ghorofa (high heels)
- Pete, mkufu, shanga n.k.
- Vibanio vya nywele
- Kupaka wanja, rangi ya midomo na rangi ya kucha

### 4.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji na usagaji.
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau bendera ya Taifa.
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani ndani na nje ya shule.
x. Kutoa mimba
xi. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi.
xiii. Kuwa na simu ya mkononi. Mawasiliano kati ya mzazi/mlezi yatafanyika kwa kupitia mkuu wa shule, makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi na si vinginevyo.

### 4.2 ANGALIZO KWA MZAZI/MLEZI

(i). Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, hivyo inakuwa na mihula mirefu miwili na mifupi miwili kwa mwaka. Mzazi/mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati shuleni, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.

(ii). Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia Mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya Malezi. Mwanafunzi **haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni**.

(iii). Shule haina utaratibu wa kuwaona wanafunzi isipokuwa mzazi ataitwa na uongozi wa shulekama kuna ulazima wa kufanya hivyo.

(iv). Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.

(v). Mzazi/mlezi kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apotezeutulivu wa maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.

(vi). Shule ina utaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mbali kipindi shule inapofunga. Hivyo mzazi/mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufunga.

(vii). Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.

(viii). **Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa Muuguzi wa Shule. Hii itarahisishia shule kumhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumhudumia. Usifiche ugonjwa, utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yako**

(ix). Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme. Akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.

(x). Shule itakapokuwa imefunga, likizo zote **mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofungua atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi) moja kwa moja kuja shuleni**. Atakayekiuka utaratibu huu atarudishwanyumbani kwa gharama zake.

(xi). Mwanafunzi haruhusiwi kuja na kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu, hata kama anatoka mbali. **AKIJA NAVYO ATAFUKUZWA SHULE (ATAFUTWA SHULE MARA MOJA).**

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kimamilifu**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NASULI**

……………………………………….

**MWL.DAFROSA CHILUMBA**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NASULI
NAMTUMBO

**Kiambata ‘’A’’**

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NASULI

**A. Sehemu ya mwanafunzi**

Mimi…………………………………………………………………………………

Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza kwa mwaka……………….katika shule ya sekondari Nasuli na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na Nchi.Ninaahidi kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai.Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni…………………………………………………………

……………………………………………….

………………………………………………

………………………………………………

Sahihi………………………………………. Tarehe……………………………………

**B. Sehemu ya Mzazi/Mlezi**

Mimi…………………………………………………………………….ninakubali

Mtoto wangu………………………………………………. Kuchukua nafasi ya kuingia Nasuli sekondari kidato cha kwanza mwaka…………………………Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.Pia nakiri kukubaliana na sheria,kanuni za shule pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni

………………………………………………………….

…………………………………………………………..

…………………………………………………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi,ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi
Sahihi………………………………………………………………
Tarehe…………………………………………….

**Kiambata ``B''**

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina lako kamili kama lilivyotumika darasa la saba ……………………………………
2. Shule ya msingi uliyo soma…......................................……………………………..
3. Dini yako /dhehebu……………………………………………………..…………….
4. Jina kamili la baba mzazi/ mlezi……………………………………………………….
   Kazi yake………………………………………………………………………………
   Anuani kamili ya baba mzazi/mlezi……………...…………………………………….
   Na.yake ya simu ya mkononi…………………..………………………………………
   Na. yake ya simu ya mezani…………………………………………………………...
   Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi: Mkoa…………….… Wilaya……………………
   Tarafa……………………………………Kata……………………………………….
   Kijiji/ Mtaa………………………….

5. Jina kamili la mama mzazi /mlezi…………………………………………………………
   Kazi yake……………..……………………………………………………………..
   Anuani kamili ya mama mzazi / mlezi……………………….………………………
   Na. yake ya simu ya mkononi………………………………………………………..
   Na. yake ya simu ya mezani………………………………………………………….
   Mahali anakoishi mama mzazi /mlezi…………………………………………………
   Mkoa……………………………Wilaya………………………………………………
   Tarafa…………………………………kata…………………………………………
   Kijiji / Mtaa……………………………………..

**FOMU MAALUM INAYOONYESHA TAARIFA ZA NDUGU WA JIRANI NAMWANAFUNZI**

Ndugu wa karibu na mwanafunzi: Hakikisha unaandika majina mawili na anwani zao.Hii inasaidia shule kutoa taarifa endapo tatizo litatokea . Hatutaki majina ya ndugu wa bandia.

1. (a) Jina :_____________________________________________

   (b) Uhusiano: ____________________________________________
   (c) Anwani:______________________________________________
   (d) Namba ya Simu:________________________________________

Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji__________________________________Muhuri
Namba ya simu ..............................

2. (a) Jina :______________________________________________

   (b) Uhusiano: ____________________________________________
   (c) Anwani:______________________________________________

   (d) Namba ya Simu:_________________________________________

Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji_________________________________Muhuri
Namba ya simu ..............................

Saini ya mzazi: _________________________

Tarehe: ___________________________

**Kiambata "C"**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT `S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**

NASULI SECONDARY SCHOOL,

POBOX 21,

NAMTUMBO,

30/03/2022

DISTRICT MEDICAL OFFICER,

POBOX………………………,

Dear Sir / Madam.

**Re: A REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine Mr. /Miss …………………………………………………..as to his /her physical and mental fitness for admission as a Form one student at Nasuli secondary school in the year 2021.

Yours sincerely,

……………………………………….

DAFROSA C. CHILUMBA

THE HEADMISTRESS

---

The Headmistress,

I have examined Mr/ Miss…………………………………………as shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary education.

1. Vision with /without glasses. Right………………………. Left………………

2. Blood pressure……………………… Haemoglobin……………………………

3. Hearing………………………………………………………..

4. Urine (a) …………………………………………………….

5(a) Venareal diseases ………………………………….. (b) Bilharzia……………………

6. Pregnancy………………………………………………………..

7. Neurosis…………………………………………………………

8. Is there any abnormality of?

(a) The heart…………………………………….. (b) Lungs…………………

(b) The spleen……………………………………………….

9. Are there any serious diseases e.g. Leprosy, epilepsy, asthma, diabetes etc.
……………………………………………………………………………………………………………………………

Any comments………………………………………………………………………………

Date...................................................... Signature of Medical officer ……………………………………


Station……………………………… Designation…………………………………………

**Kiambata "C"**

Rangi za uniform, Sketi, Shamba dress na Sweta


sketi






Shamba dress





# ORODHA YA VITABU

## 1. HISTORY

- Edward John (2011), **Advanced Learners History Form 5 and 6**. Oxford University Press (T) LTD.
- Shibitali & Tumaini (2011) **Recent Historical Surveys**. Dar es Salaam, Shibitali & Sons Publishers. (1&2).
- Mastering of History Book One and Two, Advanced Learners History for Form 5 and 6.
- Saleh Yassin, **Essentials in Advanced Level History Paper 1 & 2**. Ahmadiyya Printing Press.
- Mwl. Kato A.K **Mastering Advanced Level History**. Mweas Book Publishers and Suppliers Mwanza Tanzania.

## 2. PHYSICS

- **Advanced Level Physics, 7$^{th}$ Edition** by Nelkon and Parker.
- S. Chand's **Principles of Physics for Class XI** by V.K Mehta & Rohit Mehta.
- S. Chand's **Principles of Physics for Class XII** by V.K Mehta & Rohit Mehta.
- **A Level Physics, 4$^{th}$ Edition** by Roger Muncaster.
- **Advanced Physics, 5$^{th}$ Edition** by Tom Duncan.
- **Fundamentals of Physics, 5$^{th}$ Edition**, by Halliday Resnick Walker.
- **Electronics for Today and Tomorrow, 2$^{nd}$ Edition** by Tom Duncan.

## 3. CHEMISTRY

- S.K SAIN (2016) **Conceptual Chemistry for Class XI and XII**, S. Chand School Books.
- A. Bahl, B.S. Bahl & G.D Tuli (2012) **Essential of Physical Chemistry**, S.Chand & Company Pvt. Ltd.
- N.K. VERMA, S.K KHANNA & B. KAPILA (2012**) Comprehesive Chemistry Volume I & II for Class XII** , Laxmi Publication (P) Ltd Golden Home New Delhi.
- G.D Tuli & R.D MADAN (2011) **Advanced Inorganic Chemistry**, S. Chand & Company Ltd.

## 4. BIOLOGY

- Taylor (D.J), **Biological Science 3$^{rd}$ Edition**
- Glenn G et al (1999), **New Understanding Biology For Advanced Level, 4$^{th}$ Edition**, Oxford University Press.

## 5. GEOGRAPHY

- **Physical Geography in Diagrams For Africa** (R.B. Bunnett).
- **Practical Geography for Africa** (John M. Pritchard).
- **Physical Geography** (D.T. Msabila).
- **Human and Economic Geography** (G.C. Morgan).
- **Geography An Integrated Approach** (David Waugh).
- **Principles of Physical Geography** (F.J. Monkhouse)
- **Atlas**
- **Lanforms in Africa** (Collin Buckle)
- **General Geography** (R.B. Bunnet)

## 6. GENERAL STUDIES

- **Understanding General Studies for Advanced Level** by Joannes Bigirwamungu and Sospeter M. Deogratias.
- **General Studies for Advanced Level Certificate Form Five and Six** by Richard R.F Mbalase.

## 7. ECONOMICS

- Dr H.L. Ahuja (2008**), Principles of Microeconomics 20$^{th}$ Revised Edition** S. Chand & Company Ltd.
- Dr H.L. Ahuja (2019), **Advanced Economic Theory**, Chand & Company Ltd.
- Dr K.K. Dewett (2015), **Modern Economic Theory Revised Edition**, S. Chand Publishing.
- Ddumba Ssentamu J (2004), **Basic Economic for East Africa 1$^{st}$ Edition** Fontain Publishers, Kampala Uganda.
- Tayebwa B.M. Bernard (2011) **Basic Economics, 5$^{th}$ Edition**, Genuine Publishers and Consultants Ltd.

**8. ENGLISH LANGUAGE**

**(a) PLAYS**

- Betrayal In the City – Francis Imbuga
- I Will Marry When I Want – Ngugi wa Thong'o and Ngugi wa Mirii.
- The Bride – Austine Bukenya.
- Lwanda Magere – Okoiti Omtatah.
- An Enemy of The People – Henrick Ibsen
- Black Mamba – John Ruganda

**(b) NOVELS**

- Encounters From Africa – Macmillan Education Limited
- The Beautiful Ones Are Not Yet Born – Ayi Kwei Armah
- A Man of The People – Chinua Achebe
- Divine Providence – everin N. Ndunguru
- The Rape of The Pearl – Magala Nyayo
- Vanishing Shadow – Namige Kayondo
- His Excellencey The Head of State – Danny Sato
- A Season of Waiting – David Omowale

**(c) POETRY**

- Selected Poems – Tanzania Institute of Education (TIE)
- The Wonderful Surgeon and Other Poems – Charles MLoka

**OTHER ENGLISH LANGUAGE BOOKS**

- ADVANCED LEVEL ENGLISH, A PRACTICAL APPROACH 2nd EDITION – Nicholous Asheli.
- OXFORD ADVANCED LEVEL DICTIONARY 8th EDITION
- ADVANCED ENGLISH FORM 5 AND 6, 1st EDITION – OXFORD UNIVERSITY PRESS, John J.
- ENGLISH PHONETICS AND PHONOLOGY – Peter Roach.
- ADVANCED LEVEL LITERATURE FORM 5 AND 6 – Godfrey Rulta Bukagile.m